

Annual Report 2020
Ripoti ya Mwaka 2020



A Review of the Last Year
Mapitio ya Mwaka Uliopita

Empowering a New Generation
Tunawezesha Kizazi Kipyta

www.kijana-kwanza.org

Contents

Yaliyomo

3

Welcome to Kijana Kwanza

Karibu Kijana Kwanza

4

UK Chair's Statement

Kauli ya Mwenyekiti kutoka Uingereza

5

TZ Chair's Statement

Kauli ya Mwenyekiti kutoka Tanzania

6

UK Director's Statement

Kauli ya Mkurugenzi kutoka Uingereza

7

Kijana Kwanza in Numbers

Kijana Kwanza Kwenye Takwimu

8

The House

Makazi

9

Child & Student Sponsorship

Ufadhili wa Mtoto na Mwanafunzi

9–10

Programmes 1 & 2

(Community Sponsorship Programme)

Mpango wa 1 na wa 2

(Mpango wa Ufadhili Jamii)

11

Programme 3 (Youth Development)

Mpango wa 3 (Maendeleo ya Vijana)

13

Extra-Curricular & Informal Learning

Mtaala wa Ziada na Elimu isiyo Rasmi

14

Programme 4 (Vocational Training)

Mpango wa 4 (Mafunzo ya Ufundis)

15

Study Cafe & Computer Classes

Mkahawa wa Kusomea

& Darasa la Kompyuta

16

Community Events & Short Courses

Shughuli za Kijamii & Kozi za Muda Mfupi

17

Grants & Interest-Free Loans

Ruzuku na Mkopo Usio na Riba

18–20

Campaigns

Kampeni

21–23

Other Updates

Matukio Mengene

24

Acknowledgements

Shukrani

Welcome to Kijana Kwanza

Karibu
Kijana Kwanza



Kijana Kwanza (Young People First) is a child and youth development charity that seeks to empower a new generation of Tanzanians to become engaged, globally aware and economically independent citizens.

We achieve this by providing a safe environment for children and young people to grow, stay healthy and access formal learning, vocational training and life skills. We also support families to develop economically and provide for their own children.

Our goal is for children and young people to acquire the means and abilities to become leaders, activists and change-makers. Not only will they benefit themselves but also their immediate and extended families, their local villages and communities, and society at large.

Address:

PO Box 261, Ghalla Road, Moshi, Tanzania

Telephone/WhatsApp:

+255 754 544 203

Email:

admin@kijana-kwanza.org

Kijana Kwanza (Young People First) ni taasisi inayotoa msaada kwa watoto na vijana yenye lengo la kuwezesha vijana hao kuweza kujishughulisha, kuwa na uelewa chanya wa mwenendo wa dunia na kuwa na uchumi wa kujitegemea.

Tunaitimiza hili kwa kuwapatia watoto na vijana mazingira mazuri ya kukua, kuwa na afya njema na kuwawezesha kupata elimu rasmi, elimu ya ufundi na elimu ya stadi za maisha. Pia tunasaidia familia maskini kukuwa kiuchumi ili kuweza kusaidia watoto wao.

Shabaha yetu ni kuandaa watoto na vijana kupata njia na uwezo wa kuwa viongozi bora, wanaharakati na waleta mabadiliko. Hawatanufaika wao wenywewe tu bali na familia zao na watu wao wa karibu, vijiji vyao na jamii zao kwa ujumla.

UK Chair's Statement

*Kauli ya Mwenyekiti
kutoka Uingereza*



It has been a challenging year for people across the world and I have experienced this first-hand in my day job as a medical practitioner in the National Health Service (NHS). Yet, in those most desperate moments, it has been comforting to receive pictures, stories and anecdotes of the children and young people that Kijana Kwanza is supporting in Tanzania.

I have been truly impressed to witness the speed and strength with which Kijana Kwanza has embraced new opportunities to improve the life chances of young people. In 2 years, a basic shelter for 5 orphaned children has emerged to become a lifeline for hundreds, if not thousands, who have benefited in large and small ways from the array of services offered by the charity. I invite you to read through this report to experience, in short, the organisation's achievements over the last year.

I would like to extend my sincere gratitude to all our staff and volunteers in Tanzania and to the UK Director, Mohammed Mamdani, for his leadership and stewardship of the charity.

Dr Mohammed Abdul Latif

Kimakuwa ni kipindi kigumu cha mwaka kwa watu wote duniani na mimi mwenyewe nimeshuhudia kwa ukaribu zaidi nikiwa kazini kwangu kama mtabibu katika kituo cha National Health Service (NHS) hapa Uingereza. Licha ya kuwa katika kipindi cha kukata tama, nimekuwa nikifarjika sana ninapoziona picha, hadithi na simulizi kutoka kwa watoto na vijana ambao wanafadiliwa na Kijana Kwanza nchini Tanzania.

Nimekuwa nikfurahishwa kushuhudia uwezo na kasi ambayo Kijana Kwanza imeonyesha kwa kufungua milango ya fursa mpya kwa vijana kuwa na nafasi nyininge katika maisha yao. Kwa miaka miwili, malazi ya msingi kwa yatima watano yamekuja kuwa mstari wa maisha kwa mamia, kama sio maelfu, ambao wamenufaika kwa kiasi kikubwa au kidogo kutokana na huduma itolewayo na taasisi ya Kijana Kwanza.

Nakualika kusoma ripoti hii ili ushuhudie kwa kifupi mafanikio ambayo taasisi imeyapata kwa mwaka uliopita.

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wafanyakazi wetu nchini Tanzania na pia kwa Mkurugenzi wa Uingereza, Mohammed Mamdani, kwa uongozi wake bora na usimamizi imara katika taasisi.

Dr Mohammed Abdul Latif

TZ Chair's Statement

*Kauli ya Mwenyekiti
kutoka Tanzania*



Kijana Kwanza is more than an organisation that helps people. Rather, it is a community of staff, volunteers and young people, who are committed to changing society for the better.

Each of the children and students who are sponsored or supported by Kijana Kwanza are not simply recipients of aid. They are part of our family – and in particular, I consider them as my own family. My wife, Hadija, and I live on-site at the shelter with our children, alongside the children and young people who have been entrusted to our care. Our door is always open to anyone who needs our help, advice or guidance. This is the culture we have created at Kijana Kwanza, and it is one that I share with my staff and volunteers, who work so hard to bring out the best in people.

As a Tanzanian, I am very touched by the generosity of people across the world – many of whom will have never visited Tanzania – who have reached out to help our children and young people.

Thank you for remembering us and we welcome you to visit us in Tanzania as our guests.

Mujibu Idrisa Abeid

Kijana Kwanza ni zaidi ya taasisi inayowasaidia watu. Badala yake ni jumuiya ya wafanyakazi, wanaojitolea na vijana ambao wamejidhatiti kuhakikisha jamii inapata mabadiliko chanya.

Kila mwanafunzi anayefadhiliwa au kusaidiwa na Kijana kwanza sio tu ni mpokea misaada kwetu bali ni moja ya familia yetu na hasa mimi binafsi nawachukulia kama familia yangu. Mimi na mke wangu Hadija, tunaishi pamoja na wanafunzi ndani ya makazi ya taasisi, hivyo tunawalea na kuwatunza vijana wetu katika malezi bora. Milango yetu ipo wazi kwa yejote anayehitaji msaada, ushauri au mwongozo wa aina yoyote kutoka kwetu. Huu ni utamaduni tuliojijengea katika taasisi yetu, na ni utamaduni huo ambao tunashirikiana na wafanyakazi wote kuhakikisha tunatoa huduma bora kwa jamii.

Kama Mtanzania, nimeguswa sana na wema wa watu mbalimbali duniani ambao wengi wao hawajawahi kutembelea Tanzania lakini wamejitoa kusaidia watoto na vijana wetu.

Asante kwa kutukumbuka na tunakukaribisha kututembelea Tanzania kama wageni wetu.

Mujibu Idrisa Abeid

UK Director's Statement

*Kauli ya Mkurugenzi
kutoka Uingereza*



I still recall those early days when our shelter housed just 5 children: Christian, Hassan, Riziki, Said and Erick. At the time, our premises seemed too large for our needs and we were desperate to raise the funds so that we could offer shelter to more young people. Fast forward 2 years, and now our concern is how to choose between a child with no living parents and a child who has been abandoned by his or her parents.

I now spend most of my time in Tanzania, living and working alongside our staff, volunteers and young people, which has given me a real insight into the local culture. Yet when it seems that I have seen the worst of poverty, another home-visit or another encounter, quickly challenges my assumptions.

The last year has seen a major expansion of our work. Aside from sheltering vulnerable children, we provide numerous services that seek to tackle child and youth disadvantage in different ways, from informal learning to microfinance and community housing. These priorities are set by staff and volunteers on the ground, who identify needs, innovate and pilot new interventions. I hope that this report will also create new understanding of these initiatives.

I am sincerely grateful to all our donors for listening to the stories of our children and young people and coming to their aid. I am also very grateful to the UK and Tanzanian Boards of Trustees for their advice and guidance and to the Tanzanian staff and volunteers for hosting me in Moshi, Tanzania.

Mohammed S Mamdani

Bado nazikumbuka zile siku ambazo Makazi yetu yalikuwa yana malazi ya watoto 5 tu ambaa ni: Christian, Hassan, Riziki, Said and Erick. Kwa muda huo, majengo yetu yalioneckana makubwa kuliko mahitaji yetu kwahiyoo tulihitaji kupata fedha kwa ajiri ya kuweza kuwapatia makazi vijana wengine zaidi. Miaka miilli imepita haraka, na sasa wasiwasi wetu ni jinsi gani ya kuchagua kati ya watoto wasiokuwa na wazazi na watoto ambaa wametelekezwa na wazazi wao.

Kwa sasa natumia muda mwingi nchini Tanzania, kuishi na kufanya kazi pamoja na wafanyakazi na vijana wetu. Hii imenipa taswira halisi ya utamaduni wao. Wakati mwingine napata wasaa wa kutembelea jamii mtaani na kuona hali ya umaskini illokithiri kutoka kwa baadhi ya wananchi ninaokutana nao. Kwa haraka hali hii inatia changamoto dhana yangu.

Mwaka uliopita tumepanua sana kazi zetu, mbali na kuwapatia makazi watoto walio katika mazingira magumu, tumetoa huduma nyngi ambazo zillenga kutatua shida za watoto na vijana wasiojiweza kwa njia mbalimbali - kutoka kwenye elimu rasmi mpaka uwezekaji wa mtaji mdogo na makazi ya kijamii. Hivi vipaumbele viliwekwa na wafanyakazi papo hapo kwa kutambua mahitaji, kuanzisha na kutengeza mipango mipya. Nina imani kuwa hii ripoti itatengeneza pia uelewa wa hiyo mipango.

Natoa shukrani zangu za dhati kwa wafadhili wetu wote kwa kusikiliza simulizi za watoto na vijana wetu na kujitoa kuwasaidia kwa moyo wote. Pia ninawashukuru sana Wajumbe wa Bodii ya Udhamini nchini Uingereza na Tanzania kwa ushauri na muongozo, na pia natoa shukrani zangu kwa wafanyakazi wa Kijana Kwanza Tanzania kwa kuwa wenyeji wangu ndani ya Moshi, Tanzania.

Mohammed S Mamdani

Kijana Kwanza in Numbers

*Kijana Kwanza
Kwenye Takwimu*

**46**

Sponsored
Students

*Wanafunzi
Waliofadhliliwa*

161

Young People
Have Learned To
Use a Computer

*Vijana Waliojifunza
Kutumia Kompyuta*

406

Young People
Visited the
Study Café

*Wanafunzi Waliotumia
Mkahawa wa Kusomea*

6,198

Kilometres
Travelled by our
School Bus

*Kilomita Lilizotembea
Basi la Shule*

200

Desks Sponsored
at our
Local School

*Madawati Yaliyotolewa
Shule ya Kata*

2,400

Bottles of Soap
Distributed
During Lockdown

*Chupa za Sabuni
Zilizotolewa Kipindi cha
Zuio la Kutoka Nje*

30

Goat Herds
Provided to Low-
Income Families

*Makundi ya Mbuzi
Yaliyotolewa kwa Watu
Wenye Kipato cha Chini*

36,135

Meals Served at
Kijana Kwanza

*Milo Iliyotolewa
Kijana Kwanza*

150

Mattresses
Distributed to
Flood Victims

*Magodoro Yaliyotolewa kwa
Wahanga wa Mafuriko*

27

Staff &
Volunteers

Wafanyakazi

205

Number of Grants
& Interest-Free
Loans Provided

*Namba ya Misaada na
Mikopo Iliyotolewa*

4,745

Total Direct
Beneficiaries

*Wanufaika Wote
kwa Ujumla*



Kijana Kwanza is based in 2 neighbouring urban villas at the foot of Mount Kilimanjaro, minutes away from the centre of Moshi Town. The properties provide shelter for 12 boys and 12 girls and include classrooms, a marquee for outdoor events and garden areas that include vegetable patches, fruit trees and a poultry farm of over 100 chickens.

The premises are also a welcoming and safe space for children and young people from across the community to access day-services, events and activities. In the coming year, we will expand capacity, with all our secondary school students moving to a newly renovated shelter in Rau District on the outskirts of town.

Kijana Kwanza inapatikana katika majengo mawili yaliyopo chini ya milima Kilimajaro nje kidogo ya Moshi Mjini. Haya majengo yanatoa malazi ya vijana wa kiume 12 na wakike 12 na ikihusisha madarasa, marquee kwa ajili shughuli mbalimbali na sehemu za bustani yenye mbogamboga, miti ya matunda na shamba la ufugaji lenye kuku zaidi ya 100.

Mbali na kuwafadhili wanafunzi makazi, pia inatoa ukaribisho na sehemu salama kwa watoto na vijana kutoka kwenye jamii kuweza kupata huduma za siku, matukio na kazi mbalimbali. Mwaka unaokuja tutatanua makazi, kwakuwa wanafunzi wetu wote wa sekondari watahamia katika makazi mapya yaliyopo kata ya Rau wilaya ya Moshi Vijiji.

Child & Student Sponsorship



The vast majority of our academic and welfare support for children and young people is funded through direct donor sponsorship. Kijana Kwanza facilitates a tiered sponsorship programme that reflects the differing needs and aspirations of children and young people in our community.

Programmes 1 & 2 (Community Sponsorship Programme)

Programmes 1 and 2, also referred to as the Community Sponsorship Programme, provide support for children in secondary school who live in the community. Beneficiaries of Programme 1 live with at least one parent, who is struggling to pay for the schooling and maintenance of his or her child. Meanwhile, children in Programme 2 are fostered, and live with either a member of their extended family or a non-relative. These children are normally orphaned or abandoned.

Sponsorship for Programmes 1 and 2 includes:

- School Uniform
- School Supplies
- School Meals
- Monthly Food Parcel
- Medical Insurance
- Monthly Visits from a Social Worker

Fostered children on Programme 2 also receive a clothing grant and a monthly payment to the foster parent. Additional support is also offered based on the assessed needs of the child such as help with shelter, utility bills and other essentials.

Ufadhili wa Mtoto na Mwanafunzi

Idadi kubwa ya msaada wetu wa kitaaluma na ustawi wa watoto na vijana unafadhiliwa kuitia ufadhili wa moja kwa moja. Kijana Kwanza inawezesha mpango wa ngazi za ufadhili ambao unaonyesha mahitaji na matarajio tofauti ya watoto na vijana katika jamii yetu.

Mpango wa 1 na wa 2 (Mpango wa Ufadhili Jamii)

Mpango wa kwanza na wa pili pia unajulikana kama Mpango wa Ufadhili Jamii, unatoa msaada kwa watoto wa shule za sekondari ambao wanaishi kwenye jamii. Wanaofaidika kwenye huu mpango wa 1 ni mtoto ambaye anaishi angalau na mzazi mmoja ambaye anaweza kufanya kazi, lakini bado anashindwa kutoa huduma na kusomesha mtoto. Wakati mpango wa 2 unahuisha mtoto wa hiari ambaye anaishi labda na ndugu yake mwenye familia nyingine au anaishi na asiyé ndugu yake. Hawa watoto kwa kawaida huwa ni yatima au wametelekezwa.

Ufadhili wa Mpango wa 1 na wa 2 unahuisha vitu vifuatavyo:

- Sare za Shule
- Vifaa vyá Shule
- Chakula cha Shule
- Kifurushi cha Chakula cha kila mwezi
- Bima ya Afya
- Kutembelewa na Afisa Ustawi wa Jamii kila mwezi

Watoto wa hiyari wa kwenye mpango wa 2 pia wanapata ruzuku ya nguo na malipo ya kila mwezi kwa mlezi wa mtoto wa hiari. Msaada wa nyongeza pia unatolewa kulingana na tathmini ya mahitaji ya mtoto ili kusaidia kwenye malazi, matumizi na vitu vingine vyá muhimu.

Martha's Story (Programme 1)



“I live with my parents, 3 siblings and 2 adopted brothers in two rented rooms in Pasua Ward. All 6 of us children share a single mattress and I find it very uncomfortable sleeping with the boys. We have very little money because my father is always drunk and never gives us anything. I started secondary school very late because I did not have money for a school uniform - I had to beg the neighbours to help me. I never eat lunch in school because we cannot afford school meals. Now that I have been sponsored, things are changing for the better and I hope to achieve my dream to be a primary school teacher.”

Simulizi ya Martha (Mpango wa 1)

“Naishi na wazazi wangu, wadogo zangu watatu na kaka zangu wawili wa hiyari kwenye vyumba viwili vya kupanga ndani ya kata ya Pasua. Sisi sote watoto 6 tunalala kwenye godoro moja na nilijikuta sijisikii vizuri kulala pamoja na kaka zangu wa kiume. Tunauezo mdogo wa kipesa kwa sababu baba yangu ni mlevi na hatusaidii kwa lolote nyumbani. Nilianza shule ya sekondari kwa kuchelewa kwa sababu sikuwa na pesa ya kununulia sare za shule, ilinibidi niombe msaada kwa majirani wanisaidie. Sikuweza kula chakula cha mchana shulenii kwa sababu familia haikuweza kunipa hela ya chakula cha shule. Ila kwa sasa nimepata msaada kutoka kijana kwanza kila kitu kinaenda vizuri na nina imani nitafikia ndoto yangu ya kuja kuwa mwalimu wa shule ya msingi”.

Lulu's Story (Programme 2)



“I didn't know my parents because dad died when mum was pregnant, and mum died when I was 7 months old. It is just me and my grandmother. She works on the farms but, because of her age, sometimes she cannot work. We live in a small mud hut without running water and electricity. It was only after I got sponsored that my sponsor bought me a solar light and paid for the water supply outside the house to be opened. For the first time in my life, I have hope. We get food every month and everything I need to go to school. This is a new beginning for me.”

Simulizi ya Lulu (Mpango wa 2)

“Siwajui wazazi wangu kwa sababu baba yangu amefariki wakati mama yangu akiwa na ujauzito wangu, na mama yangu alifariki nikiwa na miezi 7. Naishi mimi na bibi yangu. Bibi yangu anafanya kazi za shamba ila kwa kuwa umri wake ni mkubwa muda mwiningine hawezi kufanya kazi. Tunaishi kwenye kibanda cha udongo bila ya maji na umeme. Nashukuru nimepata mfadhili ambaye ametufungia umeme wa nishati ya jua na akalipia huduma ya maji nje ya nyumba yetu. Kwa mara ya kwanza katika maisha yangu nimepata matumaini. Tunapata chakula kila mwezi na mahitajil yote ya shule napatiwa. Huu ni mwanzo mpya wa maisha yangu”.

Programme 3

(Youth Development)

Mpango wa 3 (Maendeleo ya Vijana)

Children and young people in Programme 3 suffer multiple and complex vulnerabilities and reside permanently on-site at our shelter. These children are normally orphaned, former street children and/or victims of child labour or exploitation. Many of the girls admitted to this programme are at risk of sexual abuse, rape or early marriage.

For these children, we are responsible for all their needs including shelter, housing and schooling. We also provide an extensive programme of additional tuition during evenings and weekends, extra-curricular and recreational activities, as well as seasonal field trips and excursions. Our residential children also receive counselling and pastoral care and are encouraged to take part in regular volunteering and community service.

Watoto na vijana katika mpango wa 3 wamepitia matatizo mengi na ya tofauti tofauti mpaka kufikia kujunga nasi na kukaa moja kwa moja katika makazi yetu. Hawa watoto kwa kawaida ni yatima, watoto wa mitaani wa zamani na/au walioathiriwa na ajira za utotoni au unyonyaji. Wasichana wengi waliochukuliwa kwenye huu mpango ni wale waliokuwa kwenye hatari ya ukatili wa kijinsia, kubakwa au ndoa za utotoni.

Kwa hawa watoto, tunahusika kwa mahitaji yote ya mtoto kuanzia malazi na mahitaji ya shule. Pia tunatoa programu ya masomo ya ziada kwa jioni na siku za mwisho wa wiki, mitaala ya ziada, shughuli za kusherehekea pia na kwenda safari mbalimbali za kujifunza na kutalii. Sehemu yetu ya makazi pia wanapata ushauri nasaha na huduma ya uangalizi na kuhamasishwa kuwa na moyo wa kushiriki katika shughuli za kujitolea na kuhudumia jamii.



Patrick's Story



“After primary school I left my hometown because my father suffered a major accident and could no longer take care of me. In Moshi, I met a man who offered to look after me and take me to school. But he tricked me and treated me like a slave. He made me look after his animals and only gave me a little food and a place to sleep. When the staff at Kijana Kwanza found out about my situation, they rescued me and brought me to the shelter. Now I am free and I live in peace. I go to school and I have everything I need to become successful in life.”

Simulizi ya Patrick

“Baada ya shule ya msingi niliondoka nyumbani kwetu kwa sababu baba yangu alipata ajali kubwa na asingeweza kunihudumia. Nilivyofika Moshi, nikakutana na mtu aliyeniahidi atanisaidia na kunipeleka shule. Lakini alinidanganya na akawa ananitumikisha kama mtumwa. Alinifanya mchungaji wa mifugo yake na kunipa chakula kidogo tu na sehemu ya kulala. Wafanyakazi wa Kijana Kwanza baada ya kugundua hali yangu, wakanitoa pale na kunipa makazi mapya. Sasa hivi nipo huru na naishi kwa amani. Naenda shule na nina kila kitu ninachohitaji ili kuja kuishi maisha ya mafanikio.”

Halima's Story



“Both my parents died by the time I was 3 years old. It was my aunt who brought me up and helped me to go to primary school. Two years before I finished primary school, my aunt also passed away. Since I had no one to take care of me, I ended up living on the street. A few months later, a lady took pity on me and invited me to live with her, even though she was very poor. Since she was struggling to help, I was admitted to Kijana Kwanza. Now that I have a place at the shelter, I get everything I need. Not only do we study but we also have fun and learn new things.”

Simulizi ya Halima

“Wazazi wangu wote walifariki nikiwa na umri wa miaka mitatu. Shangazi yangu ndiye aliyenilea na kunisaidia kunipeleka shule ya msingi. Lakini miaka miwili kabla sijamaliza masomo yangu ya shule ya msingi shangazi yangu alifariki. Sikuwa na yeyote wa kunihudumia na niliishi mtaani. Miezi michache baadae, Dada mmoja alinikuta mtaani na kunionea huruma ndipo alinichukua nikaishi naye. Lakini alikuwa anakipato kidogo na alikuwa anapata shida kunisaidia. Kwa sasa nina sehemu ya kuishi, napata kila kitu ninachohitaji. Sio tu tunasoma bali pia tuna furahi na kujifunza vitu vipyta.”

Extra-Curricular & Informal Learning

Mtaala wa Ziada na Elimu isiyo rasmi



Alongside formal education, we emphasise the holistic development of the children in our care. Children are encouraged to adopt positive habits such as personal hygiene, good behaviour and regular house chores, which is rewarded through a points-based pocket money scheme.

During evenings and weekends, we deliver a regular programme of additional activities including sport, workshops, interactive games, lively debates and community service that aim to both entertain and broaden the knowledge and horizons of children and young people.

Some of the highlights of the year include:

- Bridge and tower building using spaghetti, glue and cardboard
- Setting up an email account and using social media
- A workshop on self-awareness led by Dr Edward Mwendamske from Youth Empowerment & Psychotherapy Aid Organisation (YEPAO)
- An introduction to new sports such as rugby and basketball
- A practical workshop on how to use a domestic electrical supply safely and install a back-up generator during power-cuts
- An environmental clean-up at local forests around Moshi Town
- A visit to Mawenzi General Hospital to distribute gifts for sick children
- Field trips to Chemka Hot Springs and Marangu Falls

Mbali ya elimu rasmi, tunahimiza maendeleo kiujuimla kwa watoto wote tunaowahudumia. Watoto wanafundishwa kuwa na moyo wa upendo, tabia njema, usafi binafsi, heshima na kufanya shughuli za nyumbani ambapo ufanisi wao katika haya unapimwa kwa alama ambazo zinamsaidia mtoto kupata pesa ya matumizi yake binafsi.

Kila jioni na siku za mwisho wa wiki, tunawasilisha mpango endelevu wa shughuli za nyongeza zikiwemo michezo, semina, majadiliano na shughuli za kijamii ambazo zina lengo la kuburudisha na kuongeza ujuzi na upeo wa watoto na vijana.

Baadhi ya matukio yaliyofanyika mwaka huu ni kama yafuatayo:

- *Kutengeneza daraja na mnara kwa kutumia tambi, gundi na kadibodi*
- *Kutengeneza barua pepe na kutumia mitando ya kijamii*
- *Semina ya Kujitambua ikiongozwa na Dr Edward Mwendamske kutoka Youth Empowerment & Psychotherapy Aid Organisation (YEPAO)*
- *Kutambulishwa kwa michezo mipya kama vile michezo wa raga na mpira wa kikapu*
- *Semina ya vitendo ya jinsi ya kutumia umeme wa majumbani na jinsi ya kutumia umeme wa jenereta*
- *Shughuli ya usafishaji mazingira katika maeneo ya misitu iliyopo Moshi Mjini*
- *Kutembelea Hospitali Kuu ya Mawenzi kutazama wagonjwa na kutoa zawadi kwa watoto wanaoumwa*
- *Kwenda kuzuru chemchem za maji moto chemka na maporomoko ya maji Marangu*

Programme 4 (Vocational Training)

Mpango wa 4 (Mafunzo ya Ufundzi)

With high youth unemployment in Tanzania and a growing population, our investment in professional and career-focused training is a cornerstone of our work. In the last year we have continued to sponsor 10 students at the JR Institute of Information Technology in Arusha across a wide range of disciplines including computer science, electronics, telecommunications and business administration. In December 2020, our students sat final examinations and we are now supporting them to find employment in a related industry.

As our current cohort of vocational students reach the end of their course, we have started to recruit and enrol new vocational students. Four students have already commenced courses in Clinical Medicine, Pharmaceutical Sciences and ICT with a further 16 joining in the New Year.

Kutokana na ukosefu wa ajira kuwa mkubwa nchini Tanzania na kuongezeka kwa idadi ya watu, uwekezaji wetu katika fani na mafunzo yanayolenga kazi ni msingi mkuu wa malengo yetu. Mwaka uliopita tuliedelea kuwasaidia wanafunzi 10 waliokuwa wakifadhiiliwa na taasisi yetu kusomea kozi mbalimbali kama vile Computer Science, Electronics, Telecommunications na Business Administration katika chuo cha JR Institute of Information Technology kilichopo Mkoani Arusha. Disemba 2020, wanafunzi wetu walifanya mitihani yao ya mwisho na sasa tunawasaidia kutafuta ajira kutokana na fani waliyosomea.

Kwa vile kundi la wanafunzi wa mafunzo ya ufundzi wameshamaliza kozi zao, tumeanza kusajili wanafunzi wapya wa mafunzo ya ufundzi. Wanafunzi wanne tayari wameshaanza masomo yao katika ngazi ya cheti kwenye fani za Clinical Medicine, Pharmaceutical Sciences na ICT na wengine 16 wanatarajiwa kujunga ndani ya mwaka mpya.

Kisra's Story



“I left home after primary school due to family problems and went to live with a teacher from secondary school. However, I didn't pass my Form 4 exams, so I could not proceed with my education until I got the chance to do an introductory course in computing. Finally, I discovered my passion and applied to Kijana Kwanza for sponsorship. This year, I successfully completed a Diploma in ICT and I already have a job offer at an NGO in Dar es Salaam.”

Simulizi ya Kisra

“Niliondoka nyumbani baada ya kumaliza elimu yangu ya shule ya msingi kwa sababu ya matatizo ya kifamilia na nikaenda kuishi na mwalimu wa shule ya sekondari. Kwa bahati mbaya sikufanikiwa kufaulu mtihani wa kidato cha nne, kwahiyio nikashindwa kuendelea na msomo yangu mpaka nilipopata nafasi ya kusomea kozi ya Introductory Course in Computing. Mwisho nikagundua kitu ninachopenda kufanya katika maisha yangu na nikaomba nafasi ya ufadhili Kijana Kwanza. Mwaka huu nimefanikiwa kumaliza stashahada ya ICT na tayari nimepata ajira katika shirika lisilo la kiserikali (NGO) jijini Dar es Salaam.”

Study Café



It is not unusual for some of the most deprived children to live in severely overcrowded housing, with several people sharing a single rented room, often without electricity and water supplies.

Our Study Café provides an informal, comfortable space for children to study, use our free Wi-Fi connection and access our library of school textbooks, which most children cannot afford.

Over 100 children access the Study Café every week, and we regularly run out of desks and chairs to accommodate the growing numbers. In the coming year, we plan to expand our seating capacity and construct a more robust shelter to protect against the sun and rainfall.

Computer Classes



In March 2020, we opened a fully equipped computer room with 10 stations, an overhead projector, Wi-Fi access and printing facilities. The new service offers young people from across Moshi Town the opportunity to access computer courses and drop-in facilities free of charge. Whilst the programme was forced to close during lockdown, it reopened in July 2020. On average, 28 young people successfully pass our in-house computer course on a monthly basis.

Mkahawa wa Kusomea

Ni kawaida sana kukuta watoto wanaishi katika mazingira magumu, mara nyingi unakuta watu wengi wanaishi kwenye chumba kimoja cha kupanga kisichokuwa na huduma ya maji wala umeme.

Mkahawa wetu wa kusomea unatoa elimu isiyo rasmi, sehemu nzuri ya kusomea, kutumia Wi-Fi yetu bure na kuweza kutumia vitabu vya shule vilivypo kwenye maktaba yetu ambavyo wanafunzi wengi hawawezi kuvipata kwa urahisi.

Zaidi ya wanafunzi 100 wanaweza kupata huduma ya mkahawa wa kusomea kwa kila wiki, na sio kawaida yetu kukosa madawati na viti vya kukalia kuchukua idadi kubwa ya wanafunzi wanaongezeka siku baada ya siku. Mwaka unaokuja tunampango wa kupanua ukubwa na uwezo wa sehemu ya kuka kusomea na kujenga majengo mengine imara kujikinga kwa juu na mvua.

Darasa la Kompyuta

Ndani ya mwezi wa Machi 2020, tulifungua darasa la kompyuta lenye vifaa vyote vinavyohitajika tukiwa na kompyuta 10, projekta, Wi-Fi na vifaa vya kuchapishia. Huduma hii mpya inawasaidia vijana mbalimbali kutoka Moshi Mjini kupata kozi bora ya kompyuta na vifaa vilivypo ndani bila malipo. Ingawa mpango ulilazimika kufungwa kipindi cha usitishaji wa shughuli za kawaida, ilifunguliwa tena mwezi wa Julai 2020, na wastani wa vijana 28 wameweza kufaulu kozi ya kompyuta kwa kila mwezi.

Community Events

Whilst lockdown in Tanzania restricted our planned programme of community events, prior to the pandemic we organised a football and netball tournament attended by over 900 children and young people. As restrictions were eased in July 2020, we began to open up our services and organised a series of interfaith events to build solidarity between Muslims and Christians. These included a traditional *mawlid*, celebrating the birth anniversary of the Prophet Muhammad, and a nativity play at Christmas for the local community.



Short Courses



Throughout the year, we have organised several short courses in English and communication skills for young people in the local community. Our volunteers have also helped to deliver short modules and revision sessions for vocational students who need extra help and support in completing their qualification.

In October 2020, we hosted 18 children from across 6 regions of Tanzania at Kijana Kwanza to attend an 8-week Pre-Form 1 course, which helps primary school students make a successful transition to secondary school. Eight of the most vulnerable students have also been selected for full sponsorship and will move to our shelter in January 2021.

Shughuli za Kijamii

Kipindi cha katazo la kusitisha shughuli za kawaida nchini Tanzania kilizua mpango wetu wa kufanya shughuli za kijamii zillizopangwa kufanywa. Kabla ya ugonjwa wa korona tulianada mashindano ya michezo ya mpira wa miguu na mpira wa pete yaliyohudhuliwa na zaidi ya watoto na vijana 900. Makatazo yaliyyopunguzwa mwezi wa Julai 2020, tulianza kufungua huduma zetu na kuandaa mfululizo wa shughuli za muingiliano wa imani ili kuleta umuja kati ya waisilamu na wakristo ikihusisha kusherekea kuzaliwa kwa Mtume Muhammad na kukumbuka jinsi Yesu alivyozaliwa.

Kozi za Muda Mfupi

Kwa mwaka mzima wote huu, tumeandaa kozi mbalimbali za muda mfupi ambazo ni kozi za kigereza na ujuzi wa mawasiliano kwa vijana katika jamii. Wafanyakazi wetu wamejitahidi kusaidia kuwasilisha moduli fupi na marudio ya vipindi kwa wanafunzi wa mafunzo ya ufundi ambao walihitaji msaada wa ziada kumalizia fani zao.

Mwezi wa Oktoba 2020, tulichukwa wanafunzi 18 kutoka mikoa 6 ya Tanzania kushiriki mafunzo ya wiki 8 ya kujiandaa kuingia kidato cha kwanza hapa Kijana Kwanza ambayo yanamsaidia mwanafunzi kutoka shule ya msingi kuweza kuhamia vema katika hatua mpya ya elimu ya sekondari. Wanafunzi nane kati ya wanafunzi 18 walio kwenye hali hatarishi wamechaguliwa kwa kupata ufadili wa moja kwa moja na wataamia kwenye makazi yetu Januari 2021.

Grants & Interest-Free Loans



In the last year we have distributed 198 grants and 7 interest-free loans to children, young people and their families in order for them to respond to emergencies and crises as well as more long-term investment in education and setting up small businesses. Since the poorest families lack access to finance and savings, our Emergency Fund has become an essential resource to provide relief and alleviate poverty.

Grants and loans are sometimes very small, starting from just Tsh. 25,000 (£8.50/\$11) for specialist textbooks or travel to visit a dying parent up to a maximum of Tsh. 5,000,000 (£1,700/\$2,200) to invest in a business.

Ruzuku na Mkopo Usio na Riba

Ndani ya mwaka uliopita tulisambaza ruzuku 198 na mkopo usio na riba kiasi kwa vijana cha 7 kwa ajili ya kuweza kujihudumia kwenye dharura na matatizo, pia na kwenye uwekezaji wa muda mrefu katika elimu na biashara ndogondogo. Kwakuwa familia za kimaskini wanakosa uwezo kupata pesa na kutunza, fungu la fedha la dharura limekuwa rasilimali muhimu kuwapa auheni na kupunguza umaskini kwenye hizo familia.

Ruzuku na Mikopo muda mwingine ni ndogo sana, kwa kianzio cha shilingi 25,000/= (£8.50/\$11) kwa vitabu vyta kitaalamu au kusafiri kwenda kutembelea mzazi na kufikia kiasi cha shilingi 5,000,000/= (£1,700/\$2,200) kwa ajili ya kuwekeza kwenye biashara.

Rama's Story



“I came to Kijana Kwanza in April 2020, after losing my job in Dar es Salaam due to coronavirus. I returned to Kilimanjaro Region to ask my family for help, but they rejected me. After visiting Kijana Kwanza, they agreed to provide me with boarding, meals and volunteer expenses. I took responsibility for the small shop in the Study Café and, for the first time, we made a good profit. I started feeling more confident about setting up a business and in November 2020, I was given an interest-free loan to open a small grocery store. Apart from repaying my loan, I have offered Kijana Kwanza a 10% stake in my business, so that they can continue to give business grants to other people.”

Simulizi ya Rama

“Nilikuja Kijana Kwanza mwezi wa April 2020, baada ya kupoteza kazi yangu jijini Dar es Salaam kwa sabu ya ugonjwa wa Korona. Nilirudi nyumbani Kilimanjaro kuwaomba familia yangu inisaidie lakini walnikatalia. Baada ya kutembelea Kijana Kwanza, walikubali kunipa bweni, chakula na posho ya kujitolea. Nilichukua kazi ya kuuza duka dogo lililopo kwenye mkahawa wa kusomea na ni kwa mara ya kwanza tukapata faida nzuri sana. Nilianza kujisikia kujiamini sana kuanzisha biashara yangu na mwezi wa Novemba 2020, nilipewa mkopo usio na riba kufungua duka dogo la vinywaji. Ukiacha na kulipa mkopo wangu, nimetoa ahadi ya kutoa asilimia 10% ya biashara yangu kwa Kijana Kwanza, ili waweze kuendelea kutoa ruzuku na mikopo isiyo na riba kwa watu wengine”.

Campaigns

Our seasonal campaigns respond to emerging needs in the community, with active participation of the children and young people in our care.

Desk Appeal

At the start of the academic year, our children brought to our attention the dire shortage of desks and chairs in their local school.



Kampeni

Kampeni zetu za msimu huwa zinalenga mahitaji yahitajikayo kwenye jamii, kwa ushiriki wa moja kwa moja wa watoto na vijana tunaowapa huduma zetu.

Maombi ya Msaada wa Madawati

Mwanzoni mwa kuanza kwa masomo, watoto wetu walileta maombi ya kuwepo kwa upungufu wa madawati na viti katika shule zao wanazosoma.



"It is hard for students to learn or take notes because there are not enough desks and chairs for all the children. Before class, the students are pushing each other so that they can get a place to sit. Sometimes 3 students share a single chair. Some of them bring buckets to class to sit on. It is the girls who suffer the most because they are not strong enough to fight for a desk."

Romana

"Ni vigumu kwa mwanafunzi kusoma au kunakili masomo ubaoni kwa kuwa hakuna madawati na viti kwa wanafunzi wote. Kabla ya kuingia darasani wanafunzi wanaskumana ili waweze kupata nafasi za kukaa. Wakati mwingine wanafunzi watatu wanatumia kiti kimoja, baadhi yao wanaleta ndoo darasani kwa ajili ya kukalia. Ni wasichana ndio wanapata shida sana kwa sababu wao hawana nguvu ya kupambania kupata dawati au kiti cha kukalia."

Romana

Kwa msaada wa wafadhili, tumeweza kuchangiwa £10,000/\$13,000 kufadhili madawati 200 katika shule ya sekondari Reginald Mengi.

With the support of our donors, we launched a £10,000/\$13,000 appeal to sponsor 200 desks at Reginald Mengi Secondary School.

Coronavirus Appeal

*Maombi ya Msaada
dhidi ya Ugonjwa wa
Homa Kali ya Mapafu*



As the global pandemic arrived in Tanzania, and schools went into lockdown, our children and young people played their part in raising awareness of basic hygiene. Mariam helped to produce a video on hand-washing that was viewed 49,193 times on our Swahili language Facebook channel, whilst staff and young people helped distribute 1,200 bottles of liquid soap in public spaces such as Mbwayuni Market and mosques and churches across Moshi Town. Alongside the distribution, our young people led street workshops on hand-washing and shared health information on keeping safe from coronavirus.

As lockdown restrictions eased, we distributed 100 face visors to local hospitals and 61 hand washing stations to schools.

Kipindi ugonjwa wa Homa Kali ya Mapafu umeingia Tanzania na shule zikafungwa, watoto na vijana wetu walifanya kazi ya kuelimisha njia za kujisafisha za msingi kujuzuia na huu mgojwa ndani ya jamii. Mariam alisaidia kutengeneza video ya kuonesha jinsi ya kunawa mikono kuweza kuangaliwa na watu 49,193 katika ukurasa wetu wa Facebook wa Kiswahili, wakati wafanyakazi na vijana wa Kijana Kwanza walisaidia kusambaza chupa 1,200 za sabuni ya maji katika sehemu zenye mkusanyiko kama vile soko la Mbwayuni, misikitini na makanisani ndani ya Moshi Mjini. Sambamba na usambazaji wa hivi vitu, vijana wetu waliongozo semina ya mtaa kwa mtaa kuhusiana na jinsi ya kunawa mikono na kusambaza taarifa za kiafya ili kujilinda na kujikinga dhidi ya ugonjwa huu wa Homa kali ya mapafu.

Baada ya katazo la usitishwaji wa shughuli za kawaida kupunguzwa, tulisambaza barakoa 100 katika hospitali na vifaa vya kunawia mikono 61 mashulen.

Flood Relief Appeal

*Maombi ya Msaada
wa Mafuriko*



In March 2020, heavy rainfall caused mass flooding in neighbouring villages around Moshi Town. A total of 116 homes were damaged, 20 were completely washed away and 6 people died. As soon as news reached Kijana Kwanza, our staff, volunteers and young people were at the scene helping to clear the debris and assess the needs of the local community.

Following an emergency appeal, our children packed 100 food parcels for local families, provided 150 mattresses and helped 177 children with uniform and replacement school bags and books.

Mwezi Machi 2020, mvua kubwa ilisababisha mafuriko kwenye vijiji vya jirani karibu na Moshi Mjini. Nyumba 116 ziliharibiwa, 20 zilisombwa na maji na watu 6 walifariki dunia. Baada tu taarifa kufikia Kijana Kwanza, wafanyakazi wetu na vijana walienda kwenye tukio kwenda kusaidia kusafisha uchafu na kukagua mahitaji ya wahanga.

Baada ya maombi ya dharura, watoto wetu walipakia vifurushi 100 nya chakula kwa ajili ya familia za waathiriwa wa mafuriko, pia tulitoa godoro 150 na kusaidia watoto 177 kuwanunulia sare za shule mabegi na vitabu ambavyo walipoteza kwenye mafuriko.

Other Updates

New Shelter in Rau District

In February 2020, we purchased a half-acre plot on the outskirts of Moshi Town, which includes 3 properties and garden areas. The new, purpose-built shelter, which has been renovated to a high standard, will house 28 children and provide a safe and comfortable environment for the most vulnerable in our care.

In January 2021, all our secondary school students will move to Rau, and our new school bus will ensure they have easy access to schools and facilities in town. This will also free up space at our rented properties in Moshi Town, providing additional capacity to run day-services and shelter vocational students.

We are currently working with pro-bono architects to develop the Rau site further and build new classrooms and staff accommodation.


Matukio Mengine

*Makazi Mapya
katika Kata ya Rau*

Mwezi Februari 2020, tulinunua eneo nusu heka nje kidogo ya Moshi Mjini, ambalo lilikuwa lina Nyumba tatu na sehemu ya bustani. Makazi yetu mapya yalijengwa na kubadilishwa kuwa na ubora mkubwa, ambao utachukuwa malazi ya watoto 28 na kuwapa mazingira salama na safi kwa watoto waliokabidhiwa kwetu kuwatunza.

Mwezi Januari 2021, wanafunzi wetu wote wa shule ya sekondari wataamia kwenye makazi ya Rau, na basi letu jipya litahakikisha wanaenda shule na kupata vitu mjini kwa urahisi. Hii pia itaacha nafasi kubwa katika jengo tulilipangisha Moshi Mjini na kupatia uwezo wa kutoa huduma za kila siku na makazi kwa wanafunzi wa mafunzo ya ufundi.

Kwa sasa tunafanya kazi na pro-bono architects kutengeneza zaidi eneo la ujenzi la Rau na kutengeneza madarasa mapya na makazi ya wafanyakazi.




Bonite Community Housing Development

Mradi wa Makazi ya Umma ya Bonite

The general concern about the lack of affordable housing for low-income families was further aggravated by the floods in Moshi at the beginning of the year. We were, therefore, inspired to develop community housing in the new suburbs of the town. In June 2020, we purchased a 1-acre plot that will, over the coming years, provide 20 low-rent properties for families, alongside some private housing to generate funds to invest in the organisation. This is a long-term project, but subject to fundraising, the first phase of 7 properties will be built next year.

Ukosefu wa nyumba za kupanga kwa familia maskini limekuwa ni tatizo kubwa Moshi Mjini. Janga la mafuriko mwanzoni mwa mwaka limefanya tatizo hili kuwa kubwa zaidi. Hivyo kama taasisi ikatusukuma kuanzisha Mradi wa Makazi ya Umma ya Bonite pembenzoni mwa Moshi Mjini. Ndani ya mwezi Juni 2020, tulinunua eneo la hekari moja ambalo kwenye mwaka unaokuja litatoa nyumba 20 za kupanga kwa bei nafuu, sambamba na nyumba binafsi ili kutengeneza fedha za kuwekeza kwenye shirika. Huu ni mradi wa muda mrefu, lakini kuliingiza kwenye ukusanyaji wa fedha, hatua ya kwanza zitajengwa nyumba 7 mwaka ujao.



Goat Herding Project

This year we launched a special microfinance initiative, in partnership with the Lady Fatemah Charitable Trust, to provide rural families with a small herd of goats to grow and develop into a business enterprise. The income generated through the sale of newly reared goats will help the family pay for essential education and health costs.

We initially piloted the programme with 5 families, but recognising its success, a further 25 families were included in the project. Families will also return 1 goat to the project within 2 years for distribution to another family.

In the coming year, we plan to expand the project further to over 100 families.

Mradi wa Ufugaji wa Mbuzi

Mwaka huu tulianzisha chanzo kidogo cha fedha kwa kushirikiana na Lady Fatemah Charitable Trust kuwapa familia za vijiji makundi madogo ya mbuzi kuwakuza na kuwaingiza kwenye mfumo wa biashara. Hela itakayopatikana kwenye kuuza mbuzi mpya atakayezaliwa itasaidia familia kulipa mahitaji ya shulen na gharama za afya.

Mwanzoni tulianza mpango mradi na familia 5 tu, ila baada ya kugundua kuwa kuna mafanikio baadae familia 25 zilihusishwa kwenye mradi. Familia pia zitahitajika kurudisha mbuzi mmoja kwenye mradi ndani ya miaka miwili kwa ajili ya kusambaza kwenye familia nyiningine.

Mwaka unaokuja tunampango wa kupanua mradi kwa kuzifikia familia 100 kwenye jamii.



Acknowledgements

We would like to express our sincere thanks to the following companies and organisations that have supported our work over the last year:

Shukrani

Tunapenda kutanguliza shukrani zetu za dhati kwa kampuni zifuatazo na taasisi ambazo zimetusaidia kwenye kazi zetu kwa mwaka uliopita:

Moshi Municipal Council

Lady Fatemah Chairitable Trust

Raha Foundation

Livingston Charitable Trust

A F Dahya Family Foundation

Lamabuild Ltd

TaxAssist Accountants

HMJK Architects

Hasnain Foundation

Freedom Traders

Dhanji Foundation

Lady Sumayya Humanitarian Aid Foundation

GF Foundation Ltd

Ahlulbayt Society for Knowledge (Ask)

Bilal Muslim Mission (Moshi)

Free Pentecostal Church Tanzania (Moshi)



...and 743 individual donors who contributed to our various programmes this year.

...na wafadhili binafsi 743 ambao wamechangia kwenye mipango miradi mbalimbali ndani ya mwaka huu.